Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# Kufanya Kilicho Sahihi



## Ufafanuzi kuhusu Maadili ya Utumishi wa Umma

Mei 2006

## Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ahadi yetu ni Kufanya Kilicho Sahihi | **2** |
| 2. | Mpangilio wa Ufafanuzi wa Maadili ya Utumishi wa Umma | **3** |
| 3. | Madhumuni ya Ufafanuzi wa Maadili ya Utumishi wa Umma | **4** |
| 4. | Maswali yanayoulizwa mara kwa mara na Ufafanuzi wake | **4** |
| 5. | Kufanya kilicho sahihi – Maadili ya Msingi ya Utumishi wa Umma | **8** |
| 6. | Kufanya kilicho sahihi – Maadili ya Utumishi wa Umma | **9** |
| 7. | Mambo yanayofaa na yasiyofaa kutenda | **11** |
| | Maadili ya msingi: Kuzingatia TAALUMA | **14** |
| | Maadili ya msingi: Kuwa MWAMINIFU | **19** |
| | Maadili ya msingi: Kuwa MWAJIBIKAJI | **22** |
| 8. | Kutanzua mitanziko ya kimaadili | **25** |
| 9. | Jinsi ya kutumia Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma | **29** |
| 10. | Kufanya uamuzi wa kimaadili kwa kutumia SHEKAMABI | **30** |

# 1. Ahadi yetu - Kufanya kilicho sahihi

Ili nchi iwe na maendeleo ni muhimu kwa kila mwananchi kudhamiria kufikia kiwango cha juu cha uadilifu. Hii inamaanisha kwamba tunahitaji **kufanya kilicho sahihi** daima ili kujenga imani ya watoto wetu, watumishi wenzetu na wananchi wengine.

Kama Mtumishi wa Umma, ili kufanya kilicho sahihi hapana budi kutekeleza majukumu kwa kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwajibika. Kwa upande wake, Serikali ina jukumu la kuwajengea uwezo watumishi wake ili waweze kuzingatia utaalamu wao, wawe waaminifu na wawajibike.

Ufafanuzi unaotolewa katika kitabu hiki una lengo la kusaidia uelewa wa Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma na hapana budi kusomwa pamoja na Sera, Sheria na Kanuni za nchi. Kwa kutumia maadili yaliyoainishwa kwenye Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma ufafanuzi huu unachanganua maadili ya msingi ya kuzingatia utaalamu, kuwa mwaminifu na kuwajibika.

Ufafanuzi huu una mifano itakayokusaidia kuelewa mitanziko ya kimaadili unayokabiliana nayo ili kukusaidia kufanya uamuzi kwa uadilifu. Vilevile, kama mtumishi wa umma, mwenye kuzingatia utaalamu, mwaminifu na mwenye kuwajibika ni jukumu lako daima kufanya kilicho sahihi. Ndio maana maadili haya ya msingi yanakuhusu na yanatumika kwetu sisi sote, bila ya kujali jinsia, kabila, rangi, cheo, dini au umri. Kama mtumishi wa umma wewe pia ni mlezi wa dhamana ya umma. Watu unaowahudumia wanakutegemea utekeleze majukumu yako kwa uadilifu na kwa kiwango cha juu cha uwezo wako. Hivyo una wajibu wa kuonyesha kuwa unastahili dhamana hiyo kwa kutekeleza kwa vitendo maadili ya utumishi wa umma. Hivyo ukimwona mwananchi au mtumishi anakiuka maadili ya utumishi wa umma unatakiwa utoe taarifa kwa Mamlaka husika. Serikali imekusudia kuweka utaratibu wa kupokea taarifa na malalamiko ulio dhabiti na salama kwa watoa taarifa au walalamikaji.

Endapo unahitaji ushauri zaidi kuhusu Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma au Ufafanuzi huu tafadhali wasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kama mmoja wa wanaowajibika kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Utumishi wa Umma, mimi binafsi nimedhamiria kuonyesha mfano wa kutekeleza majukumu kwa kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji. Kutokana na dhamana ya umma uliyopewa na wewe pia unatakiwa uwe mfano wa kuigwa.

**Ruth H. Mollel**
**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

## 2. Mpangilio wa Ufafanuzi wa Maadili ya Utumishi wa Umma

- Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma
  - Maadili ya Msingi: Kuzingatia taaluma
    - Kanuni ya 1: Kutoa Huduma Bora
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
    - Kanuni ya 2: Kufanya kazi kwa Bidii
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
    - Kanuni ya 3: Kutokuwa na Upendeleo
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
    - Kanuni ya 4: Matumizi Sahihi ya Taarifa
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
  - Maadili ya Msingi: Uaminifu
    - Kanuni ya 5: Uadilifu
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
  - Maadili ya Msingi: Kutimiza wajibu
    - Kanuni ya 6: Utii kwa Serikali
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
    - Kanuni ya 7: Kuwajibika kwa Umma
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano
    - Kanuni ya 8: Kuheshimu Sheria
      - Yanayofaa kutenda na Yasiofaa kutenda
      - Mifano

# 3. Madhumuni ya Ufafanuzi

Kutokana na madaraka uliyopewa kama mtumishi wa umma daima kuna uwezekano wa kufanya jambo kwa usahihi au kwa makosa. Kwa kuwa mara nyingi hatukubaliani kuhusu nini kilicho sahihi na nini si sahihi, ufafanuzi unaotolewa humu unalenga kurahisisha uelewa wa Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma kwa kuainisha mipaka ya kufanya yaliyo sahihi – yaani kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji.

Ufafanuzi huu hautofautiani na Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma na umetayarishwa ili kurahisisha kuelewa maana ya kufanya kilicho sahihi.

# 4. Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

## 4.1 Maadili ya Msingi ni nini?

Maadili ya Msingi ni viwango vya utendaji vinavyokuongoza katika kufanya kilicho sahihi. Maadili ya msingi yanawahusu wote, yaani yanakusudia kumwongoza kila mtu bila ya kujali hadhi yake katika jamii, umri, jinsia, dini au kabila. Maadili ya Msingi ambayo yanasisitiza kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji ni muhimu kwa watumishi wote wa umma.

## 4.2 Maadili ya Msingi ya Utumishi wa Umma ni nini?

Maadili ya Msingi ya Utumishi wa Umma ni kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji.

## 4.3 Kufanya kilicho sahihi maana yake ni nini?

Kufanya kilicho sahihi ni kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji.

# Maadili ya Msingi 1: Kuzingatia Utaalamu

## 4.3.1 Kuzingatia utaalamu maana yake ni nini?

Kuzingatia utaalamu maana yake ni kutoa huduma kwa viwango vya juu kabisa kwa:

- Kutoa huduma bora
- Kufanya kazi kwa bidii
- Kutokuwa na upendeleo wakati wa kuwahudumia watu
- Kutumia taarifa za kazi ipasavyo

### 4.3.1.1 Kutoa huduma bora maana yake ni nini?

Kutoa huduma bora maana yake ni kufanya kazi ya kuwahudumia wateja kwa ubora na ufanisi.

### 4.3.1.2 Kufanya kazi kwa bidii maana yake ni nini?

Kufanya kazi kwa bidii maana yake ni kufanya kwa juhudi, kasi na kwa usahihi.

### 4.3.1.3 Kutokuwa na upendeleo maana yake ni nini?

Kutokuwa na upendeleo maana yake ni kuwatendea haki wote wakati wa kuwahudumia bila ya kujali hadhi, jinsia, dini, umri, au kabila.

### 4.3.1.4 Kutumia taarifa rasmi za kazi ipasavyo maana yake ni nini?

Kutumia taarifa rasmi za kazi maana yake ni kuwa mwangalifu unapotumia nyaraka zote za kazi. Nyaraka za namna hii hazikusudiwi kuachwa ovyo au kuwafikia watu wasiohusika au kutumia kwa manufaa binafsi.

# Maadili ya Msingi 2: Kuwa Mwaminifu

### 4.3.2 Kuwa Mwaminifu maana yake ni nini?

Kuwa **mwaminifu** maana yake ni kuitunza na kuitumia ipasavyo amana uliyopewa. Mtumishi mwaminifu hutambuliwa kutokana na matendo yake:

- Kwa kufanya kazi kwa **uadilifu**.

#### 4.3.2.1 Kuwa Mwadilifu maana yake ni nini?

Kuwa **mwadilifu** maana yake ni kuzingatia ahadi yako wakati unapotoa huduma na kutimiza majukumu yako kama Mtumishi wa Umma.

# Maadili ya Msingi 3: Kutimiza wajibu

### 4.3.3 Nini maana ya kutimiza wajibu?

**Kutimiza wajibu** ni kufanya na kukamilisha jambo unalotarajiwa kulifanya. Mtumishi wa Umma anayetimiza wajibu huwa na kawaida ya kuaminiwa kutokana na matendo yake kwa:

- Kuwa **mtiifu** kwa Serikali;
- **Kuwajibika** kwa Umma; na
- **Kuheshimu sheria**.

#### 4.3.3.1 Utii maana yake ni nini?

Utii maana yake ni kuthamini na kufuata maelekezo ya nchi yako, mwajiri wako, wafanyakazi wenzako na raia wenzako.

#### 4.3.3.2 Kuwa Mwajibikaji ni nini?

Kuwa Mwajibikaji ni kitendo cha mtumishi kuchukua dhamana ya matendo aliyoyatenda ipasavyo au yale ambayo hakuyatenda ipasavyo.

#### 4.3.3.3 Heshima maana yake ni nini?

**Heshima** maana yake ni kuthamini haki na hadhi ya watu wengine.

### 4.4 Uadilifu maana yake ni nini?

Uadilifu ni uwezo wa mtumishi kuwa na maadili kama vile kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji. Haya yote hukufanya uwe mtumishi mwadilifu.

### 4.5 Maadili ni nini?

**Maadili** ni mwenendo mwema, ni vile anavyofanya mtumishi mwaadilifu, ni kufanya kilicho sahihi. Mtumishi mwadilifu, hazungumzii kinadharia tu kuhusu maadili kama kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji, bali hutenda.

### 4.6 Kufuata maelekezo maana yake ni nini?

**Kufuata maelekezo** ni kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, na Taratibu zinazotumika kwa watumishi wote. Chimbuko la sheria ambazo hueleza mambo yanayopasa kutenda na yasiyopasa kutenda ni Maadili ya Msingi ya jamii nyingi kama vile, kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji.

#### 4.6.1 Sheria ni nini?

**Sheria** ni masharti yanayowekwa katika nchi ili kutoa mwongozo wa jinsi ya kufanya mambo kwa usahihi. Sheria lazima zifuatwe na watu wote, na anayevunja sheria anaadhibiwa.

#### 4.6.2 Kanuni ni nini?

**Kanuni** ni maagizo kwa ajili ya asasi kubwa kama Utumishi wa Umma, zinazotuongoza kufanya mambo yaliyo sahihi. Kanuni hizi mara nyingi zinafafanua sheria za nchi yetu.

#### 4.6.3 Taratibu ni nini?

**Taratibu** ni maelekezo yanayotolewa kwa idara zetu ili kutuelekeza kufanya mambo yaliyo sahihi.

## 5. Kufanya kilicho sahihi – Maadili ya Msingi ya Utumishi wa Umma

Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma zinatuagiza kuwa kila Mtumishi wa Umma hana budi kufanya kilicho sahihi kwa kufuata maadili ya msingi ya kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji.

**Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma**

**Maadili ya Msingi 1: Kuzingatia Taaluma -**
**Kutoa huduma kwa viwango vya juu kabisa**

**Maadili ya Msingi 2: Uaminifu -**
**Kutunza na kutumia ipasavyo Amana uliyopewa na kutambuliwa kutokana na matendo yaliyo sahihi**

**Maadili ya Msingi 3: Kutimiza Wajibu -**
**Kukamilisha jambo unalotarajiwa kutenda**

Kufanya kilicho sahihi maana yake ni kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji. Sote tunataka kuishi katika jamii ambapo watu **wanafanya kilicho sahihi**.

# 6. Kufanya kilicho sahihi – Maadili ya Utumishi wa Umma

Kuzingatia **taaluma, kuwa mwaminifu** na **kuwa mwajibikaji** maana yake ni nini? Maadili ya Utumishi wa Umma yana kanuni za msingi nane zinazofafanua maana ya kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji. Kanuni hizo zinakuongoza **kufanya kilicho sahihi.**

Maadili ya Msingi 1
**Kuzingatia Taaluma** -
Kutoa huduma kwa viwango vya juu kabisa

Kanuni ya 1:
Kutoa huduma bora

Kanuni ya 2:
Kufanya kazi kwa bidii

Kanuni ya 3:
Kutokuwa na upendeleo wakati wa kuhudumia watu

Kanuni ya 4:
Kutumia taarifa za kazi ipasavyo

Maadili ya Msingi 2
**Uaminifu maana yake** ni kutunza na kutumia ipasavyo amana uliyopewa na Kutambuliwa kutokana na matendo kwa:

Kanuni ya 5:
Kuwa mwadilifu

Maadili ya Msingi 3
**Kutimiza wajibu maana yake**
Kufanya na kukamilisha jambo unalotarajiwa kutenda kwa:

Kanuni ya 6:
Utii kwa Serikali

Kanuni ya 7:
Kuwajibika kwa Umma

Kanuni ya 8:
Kuheshimu sheria

Ni rahisi sana kuelewa Kanuni za Maadili kama utakumbuka Maadili ya Msingi ya - **Kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji**. Ufafanuzi huu unaeleza ni kanuni gani za maadili zilizo chini ya maadili haya ya msingi.

**Watumishi** wa Umma wanaozingatia taaluma zao hutoa huduma za viwango vya juu kwa:

- **Kutoa huduma bora**
- Kufanya kazi kwa **bidii**
- Kutokuwa na **upendeleo** wakati wa kuhudumia watu
- Kutumia **taarifa rasmi za kikazi** ipasavyo

**Kutoa huduma bora** maana yake ni kufanya kazi kwa uwezo wako.

Kufanya kazi kwa uadilifu ni kufanya kazi vizuri na kwa **bidii**.

Kutoa huduma bila **upendeleo** maana yake ni kutoa huduma sawa kwa wote.

Matumizi sahihi ya taarifa maana yake ni kutumia **taarifa za kazi** ipasavyo na kuwa makini na nyaraka na kumbukumbu za siri.

Mtumishi wa Umma aliye mkweli hujenga uaminifu katika matendo yake yote kwa:

- Kufanya kazi kwa uadilifu.

**Uadilifu** maana yake ni kutimiza ahadi ulizozitoa na daima kutimiza majukumu yako kama Mtumishi wa Umma.

**Mtumishi** wa Umma anayetimiza wajibu wake anachukua dhamana ya matendo na maamuzi yake kwa:

- Kuwa mtiifu kwa Serikali;
- Kuwajibika kwa Umma; na
- Kuheshimu na kutii sheria za nchi.

**Utii** maana yake ni kuthamini na kuonyesha unyenyekevu kwa nchi yako, mwajiri wako, watumishi wenzako na raia wenzako.

**Uwajibikaji** maana yake ni kuchukua dhamana ya matendo yako kwa yale uliyoyatenda ipasavyo au yale ambayo hukuyatenda ipasavyo.

**Heshima** ni kuthamini haki na hadhi ya watu wengine.

## 7. Mambo yanayofaa na yasiyofaa kutenda

**Je Maadili ya msingi na Kanuni za Maadili pamoja na maelekezo maalumu yanayotolewa yananiwezesha kufanya yaliyo sahihi?**

Ili kurahisisha kuelewa namna ya **kufanya kilicho sahihi**, maadili ya msingi na kanuni za maadili husaidiwa na maelekezo mahususi ya mambo unayotakiwa kuyafanya na unayokatazwa kuyafanya. Maelezo haya yanajulikana kama: **Mambo yanayofaa** na **yasiyofaa kutenda.**

Kanuni za  maadili ya Utumishi wa Umma haziwezi kuorodhesha mambo yote yanayofaa na yasiofaa kutenda hivyo yameorodheshwa yale machache ambayo ni ya muhimu sana.

**Je, utafanya nini unapokabiliwa na hali isiyoelezwa katika mambo yanayofaa na yasiyofaa kutenda?**

Iwapo hali fulani haikufafanuliwa kwa ukamilifu kutoka kwenye Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma, ufafanuzi huu au kutoka katika sheria na kanuni za nchi yetu, mtumishi wa umma hana budi kurejea kwenye maadili ya msingi na **maadili ya utumishi wa umma kwa uamuzi sahihi.**

Kumbuka kuwa **kufanya kilicho sahihi** ni kuzingatia taaluma kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji hata kama hakuna sheria, kanuni au sera zitakazo kuongoza kwa maelezo zaidi.

Ni wajibu wa kila Mtumishi wa Umma kuelewa namna ya kuzingatia maadili ya msingi.

Ili kurahisisha uelewa, baadhi ya mambo **yanayofaa** na **yasiyofaa** kutenda katika Utumishi wa Umma yamefafanuliwa kwa kutumia mifano.

**Hata hivyo kama kuna jambo ambalo hutalielewa unaweza kupata ushauri kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma.**

# Maadili ya Msingi 1: Kuzingatia Taaluma

Kanuni ya **Kutoa huduma bora**
[Kipengele cha pili cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

Kudhamiria **kutoa huduma bora** maana yake ni:

1. Kuelewa, kufuata na kuheshimu maadili kama yalivyo kwenye kanuni za maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma.

2. Kuweka viwango vya juu kabisa na kujitathmini na kuwatathmini wengine kwa mujibu wa viwango hivi.

**Kutambua  na kutuza utendaji bora**
Songambele ana bidii ya kuboresha stadi zake za kazi. Mara nyingi anafanya kazi nzuri na kumaliza kazi alizopewa kwa wakati. Meneja wake haonyeshi kupongeza juhudi zake nzuri. Songambele anaanza kuhisi kukatishwa tamaa.

**Je, Meneja anamtendea haki Songambele?**
**Songambele afanye nini?**

3. Kuendelea kuboresha viwango vya huduma mara kwa mara kwa:

- Ubunifu;
- Uvumbuzi; na
- Kuimarisha maarifa na stadi.

4. Kuonyesha mfano bora wa Utumishi wa Umma kwa:

- Kuvaa mavazi yanayostahili;
- Kuepuka matumizi ya madawa ya kulevya na ulevi;
- Kuepuka kushirikiana na watu wenye tabia mbaya;
- Kuepuka tabia mbaya; na
- Kutunza afya na usafi binafsi.

**Kulewa baada ya saa za kazi**
Chembele ni Afisa Mwandamizi katika Utumishi Umma. Anapenda pombe na mara nyingi anatoka baa na wanawake tofauti tofauti akiwa amelewa. Watumishi wenzake wanakerwa sana na mfano anaoonyesha kama kiongozi katika Utumishi wa Umma.

**Je, Chembele anafanya kilicho sahihi?**
**Je, watumishi wenzake wafanye nini?**




5. Kuhimiza utendaji kazi wa pamoja kwa:

- Kuwa na mawasiliano sahihi;
- Kujiheshimu na kuwaheshimu wengine;
- Usimamizi mzuri na ushauri;
- Kuzawadia na kuadhibu pale inapopasa; na
- Utunzaji wa taarifa binafsi za watumishi kwa siri.

Kanuni ya **Bidii ya Kazi**
[Kipengele cha 4 cha Kanuni ya Madili ya Utumishi wa Umma]

Kuwa na bidii ya kazi maana yake ni:

1. Kuwa na viwango vya juu kabisa vya nidhamu katika utendaji kazi;
2. Kujitolea kutoa huduma kwa moyo kwa unaowahudumia;

**Matumizi ya Lugha chafu**
Pili ana mimba pevu. Amekaa kwa muda wa saa mbili katika foleni bila ya kupata huduma. Kila muuguzi anapompitia karibu Pili huomba huduma kwa unyenyekevu, “Tafadhali muuguzi, nadhani nakaribia kujifungua!” “Kwa hiyo, nifanyeje, si tatizo langu” Muuguzi anajibu.
**Je, Muuguzi anafanya kilicho sahihi?**
**Je, Pili afanye nini?**



**Kudumisha viwango vya juu vya utendaji**
Sara ni Mwalimu. Wakati wa saa za kazi haonyeshi bidii kazini na hafundishi ipasavyo. Sara anawaambia wanafunzi wake kuwa iwapo wanataka kufaulu mitihani yao wanahitaji saa za ziada za masomo. Baadhi ya wanafunzi wanahudhuria masomo ya ziada ya Sara baada ya kuomba fedha kutoka kwa wazazi wao.

**Je, Sara amefanya kilicho sahihi?**
**Je, wazazi wafanye nini?**

3. Kukamilisha majukumu kwa wakati;
4. Kuwa tayari kufanya kazi mahali popote; na
5. Kuwahi kazini.



**Kupoteza wakati na kutotimiza majukumu**
Chaurembo anashauku kubwa ya kuhudhuria sherehe za harusi mwisho wa wiki na hajali kazi aliyopewa. Kazi hiyo ni lazima ikamilike mwisho wa siku. Msimamizi anakwenda kuhudhuria mkutano na hakurudi tena mpaka saa kumi jioni, alipokuta kazi haijafanywa na Chaurembo hayupo.

**Je, Chaurembo anafanya kilicho sahihi?**
**Je, Msimamizi afanye nini?**

Kanuni ya **Kutoa huduma bila Upendeleo**
[Kipengele cha 5 cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

1. Kuheshimu haki za mtumishi wa umma na mwananchi mwingine yeyote, kuwa mwanachama na kupigia kura chama chochote ukipendacho.

2. Kushiriki katika shughuli za kisiasa ilimradi usionyeshe upendeleo upande wowote na kuzingatia msimamo wa utumishi wa umma.

**Kushiriki katika shughuli za kisiasa wakati wa kazi au mahali pakazi**
Sikitu na Majuto ni watumishi wa umma, wanasikia habari za mkutano wa kisiasa utakaofanyika mchana. Badala ya kuendelea kufanya kazi, Sikitu anaondoka kazini na kwenda kuhudhuria mkutano. Kabla ya kuondoka anamtaka Majuto aende nae kwenye mkutano huo.

**Je, Sikitu anafanya kinachofaa?**
**Je, Majuto afanye nini?**

3. Kuepuka kutumia wadhifa wako kama mtumishi wa umma kuwasiliana na wawakilishi wa kisiasa ili kujinasua kutokana na mgogoro wako binafsi na serikali, au kuendeleza maslahi yako binafsi kwa gharama za Serikali.

4. Kuheshimu haki za mtumishi wa umma na mwananchi yeyote katika kuabudu dini anayopenda ilimradi dini hiyo haikiuki sheria na haiathiri msimamo wa utumishi wa umma wa kutokuwa na dini na haiingiliani na majukumu rasmi ya kazi.

**Kuendeleza maslahi yako binafsi kwa gharama za Serikali**
Mwakambaya ni Ofisa Ugavi aliye chini ya uchunguzi kutokana na tuhuma za rushwa. Kwa kutumia mtandao wa marafiki wanasiasa aliokuwa nao kwa miaka mingi, anajaribu kuwashawishi maofisa Upelelezi kusimamisha uchunguzi wao katika shughuli zake.

**Je, Mwakambaya anafanya kilicho sahihi?**
**Je, wapelelezi wafanye nini?**

Kanuni ya **Matumizi Sahihi ya Taarifa**
[Kipengele cha 9 cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

Matumizi sahihi ya taarifa za kazi maana yake ni;

1. Utoaji wowote wa taarifa ya kazi hauna budi:

- Kupitia kwa Ofisa aliyeidhinishwa;
- Kuzingatia ukweli; na
- Kuheshimu usiri unaopaswa kuwepo.

**Matumizi mazuri ya taarifa za siri**
Sikujua ni Katibu Muhtasi. Binti yake anaomba kazi katika Ofisi hiyo hiyo. Sikujua anachukua maswali ya Usaili na kumpa binti yake. Mkurugenzi wa Utawala na Utumishi amesikia tetesi kuwa Sikujua amefanya hivyo.

**Je, Sikujua amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Mkurugenzi afanye nini?**

# Maadili ya Msingi 2: Kuwa Mwaminifu

Kanuni ya **Kufanya kazi kwa Uadilifu**
[Kipengele cha 6 cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

Kufanya kazi kwa uadilifu kwa mtumishi wa Umma kuna maana gani?

1. Kulinda rasilimali za umma kwa:

1.1 Kulinda fedha za umma, muda, vifaa na mali;na

1.2 Kutumia fedha za umma, muda, vifaa mali na watumishi kwa manufaa ya umma kama ilivyopangwa na Serikali.

**Matumizi mabaya ya Rasilimali za Taifa**
Matata ni Afisa Mwandamizi anayestahili gari la Serikali kwa matumizi ya kikazi tu. Matembezi, ambaye ni mhudumu, amemuona Matata mwisho wa wiki akisafirisha madumu ya maji kwa kutumia gari la ofisi.

**Je, Matata amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Matembezi afanye nini?**

2. Epuka migongano ya maslahi binafsi kwa:

2.1 Kutangaza mali na maslahi binafsi, za mke au mume na au mtoto wakati unapotakiwa kufanya hivyo na mamlaka yaliyoidhinishwa;

2.2 Kutowakilisha chombo chochote mbele ya Serikali baada ya kuacha utumishi wa umma kwa masuala uliyokuwa ukiyashughulikia wakati ulipokuwa mtumishi wa umma kwa muda usiopungua miaka miwili.

3. Kuepuka kutumia vibaya madaraka:

3.1 Kutumia madaraka bila kujali maslahi binafsi au maslahi binafsi ya wengine, na kutumia madaraka ndani ya mipaka iliyokubaliwa;

**Upendeleo wa ndugu katika ajira na matumizi mabaya ya madaraka**
Pesambili anafanya kazi katika Idara ya Ununuzi wa Vifaa.Mara nyingi anavujisha taarifa za siri za zabuni kwa makampuni yanayomilikiwa na ndugu zake wa karibu. Matokeo yake ni kwamba, mara nyingi wanaomba zabuni kwa gharama au makadirio ya chini na kupewa Kazi. Siku moja mtumishi mwenzake alimsikia Pesambili akijadili taarifa za siri za zabuni na kaka yake.

**Je, Pesambili amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Mtumishi mwenzake afanye nini?**

3.2 Kuzingatia majukumu ya kazi ya mtumishi wa ngazi ya chini au majukumu rasmi wakati wa kutoa maelekezo;

3.3 Kuepuka kutumia wadhifa uliokuwa nao zamani kushawishi kupendelewa, kupata manufaa usiyostahili au kupewa upendeleo kutoka vyombo vya umma baada ya kuacha utumishi wa umma;

3.4 Zingatia suala la zawadi kwa:

3.4.1 Kutoomba zawadi;

3.4.2 Kutotoa zawadi;

3.4.3 Kutopokea zawadi zaidi ya vitu vidogo vya Ofisi kama vile kalamu na kalenda.

**Iwapo huna uhakika kama zawadi unayopewa inaruhusiwa, ni wajibu wako kuwasiliana na Mkuu wako wa kazi au Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma.**

**Zawadi**
Wakati wa Krismas, Makelele hupokea aina mbalimbali za shajara na kalenda kutoka kwa wateja. Aidha alipokea zawadi ya simu mpya ya mkononi. Mkurugenzi huwatahadharisha watumishi wasipokee zawadi zaidi ya viandikia vya kawaida vya ofisi. Mkurugenzi alimuona Makelele akiitumia simu mpya aliyopewa.

**Je, Makelele amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Mkurugenzi afanye nini?**

3.5 Kuepuka Rushwa kwa:

Kutotumia ushawishi usiofaa au kuchukua marupurupu yasiyostahili, iwe moja kwa moja au vinginevyo kwa kuomba, kutoa au kupokea rushwa/hongo.

3.6 Kutodanganya au kutoa taarifa za uongo kwa madhumuni ya kujipatia manufaa binafsi yasiyostahili.

**Kutoa Hongo**
Masanja alikuwa na haraka ya kuwahi katika usaili muhimu. Alipitiliza kwenye taa nyekundu za barabarani, na afisa wa polisi wa usalama barabarani alimsimamisha. Ofisa huyo wa polisi alimwambia Masanja lazima aende katika kituo cha Polisi ili akalipe faini. Masanja alijua kwamba kufanya hivyo kungemchelewesha zaidi na hivyo alimpa polisi wa usalama barabarani fedha kidogo ili amwachie.

**Je, Masanja amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Ofisa wa polisi wa usalama barabarani afanye nini?**





**Kudai malipo ya baada ya saa za kazi ya uongo**
Dotto ni mfanyakazi wa Masjala mwenye familia kubwa na anahitaji fedha za kulipia ada za shule. Mara kwa mara huwasilisha fomu za madai ya malipo ya kufanya kazi baada ya saa za kazi. Hata hivyo mara nyingi jioni hukutwa na mtumishi mwenzake Tumaini, akiwa amelala fofofo mezani.

**Je, Dotto amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Tumaini afanya nini?**

## Maadili ya Msingi 3: Kuwa Mwajibikaji

Kanuni ya **Utii kwa Serikali**
[Kipengele cha 3 cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

**1. Kuwa mtiifu kwa Serikali maana yake ni:**
Kuheshimu Serikali iliyopo madarakani kwa kutekeleza sera na maelekezo ya kisheria yanayotolewa na Mawaziri na viongozi wengine.

**Utii kwa Serikali**
Sikudhani ni ofisa mwandamizi katika wizara. Waziri alimpa maelekezo ya namna ya kusaidia utekelezaji wa sheria mpya iliyopitishwa Bungeni hivi karibuni. Sheria haikuwa na tatizo, ni nzuri na haipendelei. Sikudhani alikuwa hampendi waziri na aliamua kuchelewesha utekelezaji kwa njia mbalimbali.

**Je, Sikudhani amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Waziri afanye nini?**

Kanuni ya **Kuwajibika kwa Umma**
[Kipengele cha 7 cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

1. Kutambua kuwa jukumu la msingi la mtumishi wa umma ni kuhudumia umma:

**Utumishi wa Umma ni Dhamana ya Umma**
Zawadi anataka kuendeleza usajili wa gari lake. Amekuwa akisubiri katika foleni kwa muda mrefu. Ofisa anayehusika anafanya kazi polepole sana na mara nyingi alionekana akiacha meza yake na kuzungumza na wafanyakazi wenzake kuhusu matukio ya hivi karibuni ya mpira na burudani. Ilipofika zamu yake alilalamikia ucheleweshaji wa huduma kutoka kwa yule ofisa. Ofisa huyo alimkatisha na kumwambia badala ya kushukuru kwa kuhudumiwa analaumu “Mimi nakusaidia, kwa hiyo usilalamike” alisema.

**Je, Ofisa huyo amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Zawadi afanye nini?**

2. Kuhudumia umma na mtumishi mwenzako kwa heshima, hasa makundi ya wasiojiweza, kama vile wazee, wagonjwa, watoto, masikini, walemavu na wengine walio na mahitaji maalumu.

**Kuwahudumia kwa Heshima watu walio na shida maalumu**
Mawazo ana UKIMWI na ni mgonjwa sana. Kila juma anatakiwa kwenda hospitali kwa ajili ya matibabu. Hali yake inazidi kuwa mbaya. Mara nyingi daktari amekuwa akimtelekeza kwa muda mrefu na kuwahudumia wagonjwa wengine wasioumwa sana. Ndugu yake alimlalamikia daktari kuhusu tabia hiyo. Daktari alisema kuwa katika hatua hiyo ya ugonjwa hakuwa na cha kufanya.

**Je, Daktari amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Mawazo afanye nini?**

3. Kufafanua au kutoa maelezo kwa haraka na bila upendeleo kuhusu masuala ya sheria, kanuni na taratibu.

Kanuni ya **Kuheshimu sheria**
[Kipengele cha 8 cha Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma]

Kuheshimu sheria maana yake ni:

1. Kuelewa na kutii sheria, kanuni na taratibu
2. Kutumia sheria, kanuni na taratibu wakati wa kutimiza majukumu yako
3. Kuepuka ubaguzi dhidi ya watumishi wenzako na wananchi kwa sababu zisizo za msingi.

**Ubaguzi usio na sababu za msingi**
Furaha ni Mkaguzi wa Ndani hodari na anayejua kazi yake. Yeye na wafanyakazi wenzake wengi wa kiume wanafikiriwa kupandishwa daraja. Kamati ya Ajira inakiri kuwa Furaha anaijua kazi yake kuliko wenzake lakini wakati wa usaili wajumbe wengi wanamwambia kuwa wanadhani nafasi hiyo ya ngazi ya juu haiwezi kushikwa na mwanamke.

**Je, Kamati ya Ajira imefanya kilicho sahihi?**
**Je, Furaha afanye nini?**

4. Kuepuka unyanyasaji wa Kijinsia wa aina yoyote kama vile:

4.1 Kuomba fadhila ya mapenzi;
4.2 Kujihusisha na aina yoyote ya shambulio la ngono (kusumbua na kubaka);
4.3 Matendo au maneno yasiyofaa (Utani wa mapenzi au kukumbatia);
4.4 Kuangalia picha za ngono wakati wa saa za kazi.

**Unyanyasaji wa kijinsia**
Kila mara Neema anapokwenda kwa Majivuno, ambaye ni Mkurugenzi wake, husifiwa kuhusu mavazi na mwili wake. Mara nyingi humshikashika na humkumbatia. Hali hiyo inamfanya Neema akose raha.

**Je, Majivuno amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Neema afanye nini?**

5. Epuka kuomba fadhila ya mapenzi au kutumia ngono ili kupewa upendeleo



**Fadhila ya mapenzi**
Amanda amepewa fursa na Mkurugenzi wake ya kwenda kuhudhuria mafunzo ya aina fulani muhimu Johannesburg. Hata hivyo anamwarifu kuwa atakwenda tu kwa masharti ya kufanya nae mapenzi.

**Je, Mkurugenzi huyo amefanya kilicho sahihi?**
**Je, Amanda afanye nini?**

## 8. Kutanzua mitanziko ya Kimaadili

Wakati mwingine maadili yanayotuongoza katika mChaurembo yetu hugongana au hushindana hivyo kutufanya tusiwe na uhakika wa nini cha kufanya. Katika hali kama hiyo mtu anahitajika kufanya uamuzi wa ni kipi muhimu. Kuna mitanziko mingi ya kimaadili lakini mitanziko ya kawaida sana ya kimaadili inayowakabili watumishi wa umma ni **Ukweli** dhidi ya **Utiifu**.

**MFANO WA 1: Mtanziko wa Kimaadili**
Baraka anafanya kazi katika idara moja na rafiki yake mkubwa, Maneno. Siku moja Maneno alimwambia Baraka kuwa mara kwa mara huchukua karatasi kutoka ofisini na kumuuzia mwenye duka ambaye ni jirani na nyumba yake. Alimuomba Baraka amtunzie siri hiyo. Wiki liliyofuata Msimamizi wa Baraka alimuuliza iwapo Maneno anachukua karatasi za ofisi kwa matumizi yake binafsi.

**Mtanziko ni**
**Baraka anataka awe mtiifu kwa rafiki yake mkubwa Maneno.**
**Baraka ni mtu mwadilifu na anataka kusema ukweli.**

**Je, Baraka afanye nini?**

### Kufanya maamuzi ya kimaadili kwa kutumia SHEKAMABI

Kujua namna ya kufanya maamuzi ya kimaadili kunaweza kutusaidia kutanzua Mitanziko ya Kimaadili.

Hatuna budi kujiuliza maswali manne mahususi yanayoweza kukumbukwa kwa urahisi kwa kutumia kifupisho cha **SHEKAMABI**.

Kama utajibu NDIO kwa maswali yote manne inaonyesha kwamba utafanya kilicho sahihi.

Baraka hana budi kujiuliza maswali manne yafuatayo ili kutanzua mtanziko wake wa kimaadili:

**SHE = Sheria**

***Je, kuna Sheria zozote za utumishi wa umma zinazofaa kutumika katika kumsaidia Baraka, zikiwemo zile za Maadili ya Utumishi wa Umma?***

**NDIO, Sheria zinafafanua kuwa anachofanya Maneno ni wizi wa rasilimali za umma.**

**KA = Kanuni na Taratibu**

***Je, kuna Kanuni na Taratibu za kitaifa zinazotumika katika hali ambayo Baraka anaifikiria?***

**NDIO, Kanuni zinafafanua kuwa anachofanya Maneno ni ubadhirifu wa mali ya umma.**

**MA = Maadili ya ujumla kwa utumishi wa umma na jamii**

***Je, kuna maadili ya msingi yoyote ya utumishi wa umma ya kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji yanayoelekeza maamuzi ya Baraka?***

**NDIO, Maadili yote hayana budi kumwongoza Baraka. Maneno hazingatii taaluma, si mwaminifu na wala si mwajibikaji. Baraka anataka kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji.**

## BI = Binafsi

***Je, maadili yangu binafsi – Hisia zangu za kufanya kilicho sahihi, huniongoza katika kuamua nini cha kufanya?***

**Ndio, viwango vya maadili vya Baraka vinaweza kuwa vya juu zaidi kuliko inavyotarajiwa katika utumishi wa umma. Viwango vya maadili vya Maneno vinaweza kuwa vya chini kuliko inavyotarajiwa katika utumishi wa umma.**

**Inatarajiwa kuwa viwango vya maadili vya Baraka na Maneno daima viwe sawa au kuzidi viwango vya tabia vilivyofafanuliwa na kanuni za maadili.**

## Kutanzua Mtanziko

Maneno anafanya kosa. Baraka **anafanya kilicho sahihi** na kumtolea taarifa Maneno kwa msimamizi wake. Katika hali kama hii uaminifu (maadili ya msingi – **uaminifu**) na utiifu kwa Serikali (maadili ya msingi– **kutimiza wajibu**) ni muhimu zaidi ya utiifu kwa Maneno.

**MFANO WA 2: Mtanziko wa Kimaadili**
Maganga ni Ofisa wa Mazingira anayekagua kiwanda kinachotoa ajira zinazohitajika sana kwa jamii iliyokizunguka. Maganga anakerwa kwa kugundua kuwa Menejimenti ya Kiwanda inatupa taka za sumu usiku kwenye mto ulio karibu. Menejimenti inamwambia Maganga kuwa kama watafuata miongozo ya Serikali ya utupaji taka, itakuwa ghali mno na itabidi wafanyakazi wengi waachishe kazi. Maganga anahitaji kuwasilisha tathmini ya mazingira na hana uhakika jinsi atakavyoiwasilisha.

**Mtanziko ni**
Maganga anataka kuwa mtiifu kwa jamii na hataki watu wafukuzwe kazi/wapoteze ajira zao. Maganga ni mwadilifu na anataka aeleze ukweli.

**Je, Maganga afanye nini?**

**MFANO WA 3: Mtanziko wa Kimaadili**
Bahati ni Mwendesha Mashtaka wa Serikali mwenye familia kubwa. Wakati wa uchunguzi wa rushwa amegundua waraka unaowatuhumu viongozi waandamizi wa Serikali. Anatoa taarifa hii kwa Afisa Mwandamizi wa juu zaidi anayemwagiza apoteze ushahidi unaowatuhumu viongozi hawa. Afisa Mwandamizi ana wasiwasi kuwa ajira yake na ya maofisa wenzake zitakuwa hatarini iwapo viongozi hawa wenye nguvu sana watachunguzwa. Bahati hajui la kufanya.

**Mtanziko ni**
Bahati anaifikiria familia yake na hataki kupoteza ajira yake. Bahati ni mwadilifu na anataka kueleza ukweli.

**Je, Bahati afanye nini?**

# 9. Jinsi ya kutumia kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma

## 9.1 Kupata ushauri

Kama unahitaji maelezo zaidi kuhusu maana ya kufanya kilicho sahihi, tafadhali wasiliana na Idara ya Maadili Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo ni watayarishaji wa ufafanuzi huu.

## 9.2 Kutoa taarifa ya jambo lisilofaa

Unapokutana au kushuhudia tabia isiyo ya uadilifu ni wajibu wako kama mtumishi wa umma “Kufanya kilicho sahihi” kwa kutoa taarifa katika Kitengo cha Malalamiko katika Wizara yako, Idara inayojitegemea au Wakala wako. Kila Wizara, Idara na Wakala itakuwa na Kitengo cha Malalamiko ambako malalamiko yanaweza kuwasilishwa na mtumishi kwa siri, kwa maandishi, kwa njia ya simu au barua pepe. Mara baada ya kuwasilisha malalamiko utapokea jibu.

Ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka mlalamikaji anaruhusiwa kukata rufaa dhidi ya uamuzi uliotolewa na Wizara, Idara na Wakala kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

## 10. Kufanya uamuzi wa kimaadili kwa kutumia SHEKAMABI

**Kama utajibu ndio kwa maswali yote manne kutokana na uamuzi unaokusaidia kuchukua, basi ujue kuwa unafanya kilicho sahihi.**

Jiulize maswali manne yafuatayo:

**SHE = SHERIA**

1) Je kuna Sheria zozote za Utumishi wa Umma zinazofaa kutumika katika mazingira unayofikiria zikiwemo zile za Maadili ya Utumishi wa Umma?

**KA = KANUNI NA TARATIBU**

2) Je, kuna Kanuni na Taratibu zinazotumika katika hali ambayo unaifikiria?

**MA = MAADILI YA UJUMLA KWA UTUMISHI WA UMMA NA JAMII**

3) Ni Maadili gani ya msingi ya Utumishi wa Umma ya kuzingatia taaluma, kuwa mwaminifu na kuwa mwajibikaji yanayonielekeza katika kuamua nini la kufanya?

**BI = BINAFSI**

4) Je, maadili yangu binafsi na hisia zangu za kufanya kilicho sahihi, kizuri na cha haki, huniongoza katika kuamua nini la kufanya?